**TOLEO MAALUM**

*Nyongeza ya Gazeti Rasmi la Serikali Na.121 (Miswada ya Seneti Na.13)*

JAMHURI YA KENYA

# ***NYONGEZA YA GAZETI RASMI LA SERIKALI***

## **MISWADA YA SENETI, 2025**

**NAIROBI, 22 Julai, 2025**

YALIYOMO

Mswada wa Kuwasilishwa katika Seneti— UKURASA

Mswada wa Katiba ya Kenya (Marekebisho), 2025................................ 179

IMECHAPISHWA NA KUTANGAZWA NA MCHAPISHAJI WA SERIKALI, NAIROBI

# MSWADA WA KATIBA YA KENYA (MAREKEBISHO), 2025

## Mswada wa

## SHERIA ya Bunge wa kurekebisha Katiba

.

**ULIYOTEKELEZWA** na Bunge la Kenya, kama ifuatavyo —

Anwani fupi na kuanza kutumika kwake

**1.** Sheria hii inaweza kutajwa kama Sheria (Marekebisho) ya Katiba ya Kenya, 2025 na itaanza kutumika siku kumi na nne kufuatia matangazo rasmi ya matokeo ya kura ya maamuzi yaliyoendeshwa kwa mujibu wa Ibara ya 255 ya Katiba.

Rekebisho la Ibara ya 94 ya Katiba.

**2.** Ibara ya 94 ya Katiba inafanyiwa marekebisho kwa—

(a) kuingiza vifungu vipya vifuatavyo baada ya kifungu cha 1—

(1A) Bunge litatekeleza majukumu yake ya utungaji sheria, uwakilishi na uangalizi dhidi ya kitengo tekelezi cha Serikali na vyombo vingine vya serikali kwa mujibu wa Katiba hii.

(1B) Mamlaka yote ya utungaji sheria katika kiwango cha kitaifa, yatatekelezwa na Bunge la Taifa na Seneti kwa mujibu wa Sehemu ya 4 ya Sura hii.

(1C) Katika kutekeleza mamlaka yake ya kutunga sheria, Bunge litahakikisha kwamba sheria zote zinaheshimu majukumu na mamlaka yanayotolewa kulingana na Nyongeza ya Nne ya serikali ya kitaifa na za kaunti na kuzingatia maadili ya kitaifa na kaida za utawala zilizoelezwa katika Ibara ya 10.

(b) Kuingiza kifungu kipya kifuatacho punde tu baada ya kifungu cha (2)—

(2A) Bunge linatekeleza jukumu lake la uangalizi dhidi ya—

(a) mapato ya taifa yanayotengwa kwa serikali ya kitaifa na matumizi yake; na

(b) vyombo vya Serikali na asasi nyingine za umma.

Rekebisho la Ibara ya 95 ya Katiba.

**3.** Ibara ya 95 ya Katiba inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu cha (4).

Rekebisho la Ibara ya 96 ya Katiba.

**4.** Ibara ya 96 ya Katiba inafanyiwa marekebisho kwa—

(a) kuingiza maneno “na inawakilisha maslahi maalum katika Seneti” mwishoni mwa kifungu cha (1);

(b) kuingiza vifungu vipya vifuatavyo punde tu baada tu ya kifungu cha (1)—

(1A) Seneti hujadili na kutoa uamuzi kuhusu masuala muhimu ya watu katika kaunti.

(1B) Seneti inapitisha sheria kwa mujibu wa Sehemu ya 4 ya Sura hii.

(c) kufuta kifungu cha (2);

(d) kuingiza maneno "na mapato yaliyokusanywa na " punde tu baada ya maneno "mapato yanayotokana na ugavi wa" katika kifungu cha (3); na

(e) kuingiza kifungu kipya kifuatacho punde tu baada ya kifungu cha (4)—

(5) Bunge litapitisha sheria inayoelezea utaratibu wa kuwaondoa maafisa wa Serikali katika ngazi ya kitaifa.

Rekebisho la Ibara ya 108 ya Katiba.

**5.** Ibara ya 108 ya Katiba inarekebishwa—

(a) kwa kuingiza maneno "kwa Bunge la Taifa na Seneti" mwishoni mwa kifungu cha (1);

(b) katika kifungu cha (2) kwa kufuta maneno "Bunge la Taifa" yanayojitokeza punde tu baada ya maneno "ambaye ni kiongozi katika" na kuyabadilisha kwa maneno "Bunge la Taifa au Seneti";

(c) katika kifungu cha (3) kwa kufuta maneno "Bunge la Taifa" yanayojitoza punde tu baada ya maneno "ambaye ni kiongozi katika" na kuyabadilisha kwa maneno "Bunge la Taifa au Seneti";

(d) kwa kuingiza kifungu kipya kifuatacho punde tu baada ya kifungu cha (4)—

(5) Mpangilio ufuatao wa ukuu ndio utazingatiwa katika Seneti —

(a) Spika;

(b) kiongozi wa Chama cha Walio Wengi; na

(c) kiongozi wa Chama cha Walio Wachache.

Rekebisho la Ibara ya 109 ya Katiba.

**6.** Ibara ya 109 ya Katiba inafanyiwa marekebisho kwa kufuta vifungu vya (2), (3), (4) na (5) na kuvibadilisha na vifungu vipya vifuatavyo —

(2) Mswada unaweza kuwasilishwa na mbunge au kamati katika Bunge la Taifa au Seneti.

(3) Mswada unaweza kuanzia katika Bunge la Taifa au Seneti, lakini Mswada wa kukusanya mapato ya kitaifa unaweza kuanzishwa katika Bunge la Taifa.

(4) Wakati Mswada umepitishwa na Bunge la Taifa au Seneti, Spika wa Bunge husika atauwasilisha kwa Spika wa Bunge hilo lingine ili kuwasilishwa, kujadiliwa na kupitishwa.

(5) Mswada utawasilishwa tu kwa Rais ili kupatiwa kibali baada ya kupitishwa na Bunge la Taifa na Seneti.

(6) Katika muda usiozidi siku saba baada ya Mswada kupitishwa na Bunge la Taifa na Seneti, Spika wa Bunge linaloanzisha mswada, atauwasilisha kwa Rais—

(a) Mswada huo, ili kupatiwa kibali na kuchapishwa; na

(b) Cheti kilichotiwa saini na Maspika wote wawili kinachoidhinisha kwamba Mswada huo umepitishwa na Bunge la Taifa na Seneti kuambatana na Ibara hii.

Rekebisho la Ibara ya 110 ya Katiba.

**7.** Katiba inafanyiwa marekebisho kwa kufutilia mbali Ibara ya 110.

Rekebisho la Ibara ya 111 ya Katiba.

**8.** Katiba inafanyiwa marekebisho kwa kufutilia mbali Ibara ya 111 na kuibadilisha na Ibara mpya ifuatayo—

**Utaratibu wa Miswada ya Ugavi na ya Kuidhinisha Matumizi**

**111.** (1) Mswada wa ugavi unaweza kuanzia katika Seneti lakini Bunge la Taifa linaweza kupendekeza na kupitisha marekebisho kwenye Mswada huo.

(2) Mswada wa kuidhinisha matumizi unaweza kuanzia katika Bunge la Taifa, lakini Seneti inaweza kupendekeza na kupitisha marekebisho kwenye Mswada huo.

(3) Kwa kuzingatia kifungu cha (1) na cha (2), pale ambapo Bunge linalopokea linapofanyia marekebisho Mswada wa ugavi au wa kuidhinisha matumizi, Bunge linaloanzisha linaweza kubatilisha marekebisho kwa uamuzi unaoungwa mkono na angalau—

(a) thuluthi mbili ya vikoa vyote vya kaunti katika Seneti; au

(b) thuluthi mbili ya wabunge katika Bunge la Taifa.

(4) Mswada wa ugavi au wa kuidhinisha matumizi utawasilishwa kwa Rais ili kupatiwa kibali kwa kuambatana na Ibara ya 109(5) iwapo Bunge linaloanzisha—

(a) linakubaliana na marekebisho yaliyopitishwa na bunge linalopokea; au

(b) linabatilisha marekebisho kwa kuambatana na kifungu cha (3).

(5) Katika Ibara hii—

(a) Mswada wa ugavi una maana ya—

(i) Mswada wa Ugavi wa Mapato kwa Kaunti; au

(ii) Mswada wa Ugavi wa Mapato ya Ziada kwa Serikali za Kaunti; na

(b) Mswada wa kuidhinisha matumizi una maana ya —

(i) Mswada wa Kuidhinisha Matumizi; au

(ii) Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada.

**9.** Ibara ya 112 ya Katiba inarekebishwa— Rekebisho la Ibara ya 112 ya Katiba.

(a) kwa kufuta kichwa na kukibadilisha na kichwa kipya kifuatacho—

**Kushughulikia Miswada**

(b) katika kifungu cha (1) kwa kufuta usemi tangulizi na kuubadilisha kwa usemi upya ufuatao—

(1) Kwa kuzingatia Ibara ya 111, iwapo Bunge moja linapitisha Mswada na Bunge hilo lingine —

(c) katika kifungu cha (2) kwa kufuta aya ya (a) na kuibadilisha na aya mpya ifuatayo—

(a) linapitisha Mswada kama ulivyorekebishwa, Mswada utawasilishwa kwa Rais ili kupatiwa kibali kwa kuambatana na Ibara ya 109; au

**10.** Ibara ya 113 ya Katiba inarekebishwa kwa— Rekebisho la Ibara ya 113 ya Katiba.

(a) kufuta kifungu cha (3) na kukibadilisha na kifungu kipya kifuatacho—

(3) Iwapo Mswada unaopendekezwa na kamati ya usuluhishi utaidhinishwa na Bunge la Taifa na Seneti , Mswada huo utawasilishwa kwa Rais ili kupatiwa kibali kwa kuambatana na Ibara ya 109.

(b) Kuingiza kifungu kipya kifuatacho punde tu baada ya Kifungu cha (4) —

(5) Ibara hii haitatumika kwa Mswada wa ugavi au wa kuidhinisha matumizi kwa mujibu wa Ibara ya 111.

**11.** Katiba inarekebisha kwa kufutilia mbali Ibara ya 114. Kufutilia mbali Ibara ya 114 ya Katiba.

**12.** Ibara ya 115 ya Katiba inarekebishwa— Rekebisho la Ibara ya 115 ya Katiba.

(a) kwa kufuta kifungu cha (3) na kukibadilisha na kifungu kipya kifuatacho—

(3) Iwapo Bunge litarekebisha Mswada kwa kuzingatia kikamilifu pingamizi za Rais, Mswada utawasilishwa kwa Rais ili kupatiwa kibali kwa kuambatana na Ibara ya 109.

(b) katika kifungu cha (4) kwa kufuta maneno “iwapo ni mswada unaohitaji idhini ya Seneti” yanayojitokeza mwishoni mwa aya ya (b); na

(c) katika Kifungu cha (5) kwa kufuta aya ya (a) na kuibadilisha na aya mpya ifuatayo—

(a) mswada utawasilishwa kwa Rais ili kupatiwa kibali kwa kuambatana na Ibara ya 109.

**13.** Ibara ya 116 ya Katiba inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha (1) na kukibadilisha na kifungu kipya kifuatacho— Rekebisho la Ibara ya 116 ya Katiba

(1) Mswada uliopitishwa na Bunge utachapishwa katika *Gazeti Rasmi la Serikali* katika muda wa siku saba baada ya kupatiwa kibali au katika kukamilika kwa kipindi cha kupatiwa kibali kwa mujibu wa Ibara ya 115(6).

**14.** Ibara ya 157 ya Katiba inarekebishwa katika kifungu cha (2) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa” Rekebisho la Ibara ya 157 ya Katiba.

yanayojitokeza punde baada ya maneno “kwa idhini ya” na kuyabadilisha na neno “Bunge”.

**15.** Ibara ya 173 ya Katiba inarekebishwa— Rekebisho la Ibara ya 173 ya Katiba.

(a) katika kifungu cha (3) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa” yanayojitokeza punde tu baada ya maneno “kuyawasilisha kwa” na kuyabadilisha kwa neno “Bunge”; na

(b) katika kifungu cha (4) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa” yanayojitokeza punde tu baada ya maneno “makadirio hayo kuidhinishwa na” na kuyabadilisha na neno “Bunge”.

**16.** Katiba inarekebishwa kwa kuingiza Ibara mpya ifuatayo punde tu baada ya Ibara ya 199 — Rekebisho la Ibara ya 199 ya Katiba.

**Hazina ya Bunge la Kaunti**

**199A** (1) Kumeanzishwa Hazina ya Bunge la Kaunti kwa kila bunge la kaunti.

(2) Hazina hii itatumika kwa usimamizi wa bunge la kaunti na kwa malengo mengine kama hayo yanayohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya bunge la kaunti.

(3) Kila mwaka wa kifedha, bunge la kaunti litatayarisha makadirio ya bajeti ya matumizi ya mwaka unaofuata na kuyawasilisha kwa bunge la kaunti ili kuidhinishwa.

(4) Baada ya makadirio kuidhinishwa na bunge la kaunti, matumizi ya bunge la kaunti, kama yatakavyoidhinishwa na Bunge katika Sheria ya Ugavi Mapato kwa Kaunti kwa mwaka husika, yatatolewa kwenye Hazina ya Mapato ya Kaunti na fedha hizo zitalipwa moja kwa moja kwenye Hazina ya Bunge la Kaunti.

(5) Bunge la kaunti katika kila kaunti litatunga sheria ili kuelekeza udhibiti wa Mfuko huo.

**17.** Ibara ya 215 ya Katiba inarekebishwa katika kifungu cha (2) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa” yanayojitokeza punde baada ya maneno “kuidhinishwa na” katika aya ya (a) na kuyabadilisha kwa neno “Bunge”. Rekebisho la Ibara ya 215 ya Katiba.

**18.** Ibara ya 221 ya Katiba inarekebishwa— Rekebisho la Ibara ya 221 ya Katiba.

(a) Kwa kufuta kifungu cha (1) na kukibadilisha na kifungu kipya kifuatacho—

(1) Angalau miezi miwili kabla ya kukamilika kwa kila mwaka wa kifedha, Waziri anayehusika na masuala ya fedha atawasilisha kwa Bunge makadirio ya mapato na matumizi ya serikali ya kitaifa kwa mwaka wa kifedha ufuatao ili kuwasilishwa katika Bunge.

(b) Kwa kufuta maneno "Bunge la Taifa" yanayojitokeza mwanzoni kwa kifungu cha (3) na kuyabadilisha kwa neno "Bunge";

(c) Kwa kufuta vifungu vya (4), (5) na (6) na kuvibadilisha na vifungu vipya vifuatavyo—

(4) Kabla ya Bunge kuzingatia makadirio ya mapato na matumizi, kamati za Bunge la Taifa na Seneti zitajadili na kuhakiki makadirio na kutoa mapendekezo kwa Bunge la Taifa na kwa Seneti.

(5) Katika kujadili na kuhakiki makadirio, kamati hizi zitahusisha uwakilishi wa umma na mapendekezo yao yatazingatiwa wakati kamati hizi zinapotoa mapendekezo yao kwa Bunge la Taifa na kwa Seneti.

(6) Wakati ambapo makadirio ya matumizi ya serikali ya kitaifa, na makadirio ya matumizi ya Mahakama na ya Bunge yatakapoidhinishwa na Bunge, yatajumuishwa katika Mswada wa Kuidhinisha Matumizi utakaowasilishwa katika Bunge kwa kuambatana na Ibara ya 111 ili kuruhusu pesa zinazohitajika kwa matumizi kutolewa kutoka kwenye Hazina Kuu, na kuidhinisha matumizi ya pesa hizo kwa nia zilizotajwa kwenye Mswada.

**19.** Ibara ya 222 ya Katiba inarekebishwa katika kifungu cha (2) kwa kufuta maneno "Bunge la Taifa" katika aya ya (b) na kuyabadilisha kwa neno "Bunge". Rekebisho la Ibara ya 222 ya Katiba.

**20.** Ibara ya 223 ya Katiba inarekebishwa katika kifungu cha (4) kwa kufuta maneno "Bunge la Taifa" Rerekebisho la Ibara ya 123 ya Katiba.

yanayojitokeza punde baada ya neno “Wakati” na kulibadilisha kwa neno “Bunge”.

Rekebisho la Ibara ya 224 ya Katiba.

**21.** Katiba inarekebishwa kwa kufutilia mbali Ibara ya 224 ya Katiba na kuibadilisha kwa Ibara mpya ifuatayo—

**Miswada ya Kuidhinisha Matumizi ya Kaunti**

**224.** (1) Kwa msingi wa Mswada wa Ugavi wa Mapato kwa Kaunti uliopitishwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 218, kila serikali ya kaunti itatayarisha na kupitisha Mswada wake binafsi wa bajeti na wa kuidhinisha matumizi ya kila mwaka katika muundo na kwa kuambatana na utaratibu unaoelezewa katika Sheria ya Bunge.

(2) Iwapo Mswada wa Kugawa Mapato au Mswada wa Ugavi wa Mapato kwa Kaunti katika mwaka wa kifedha haujapatiwa kibali au huenda usipate kibali, mwanzoni mwa mwaka huo wa kifedha, Bunge linaweza kuruhusu kaunti kutoa fedha kutoka kwenye Hazina Kuu.

(3) Pesa zinazotolewa kwa mujibu wa kifungu cha (2)—

(a) zitakuwa kwa malengo ya kushughulikia matumizi yaliyo muhimu katika kuendesha huduma za serikali ya kaunti husika katika mwaka huo hadi wakati ambapo Mswada wa Kugawa Mapato au Mswada wa Ugavi wa Mapato kwa Kaunti utakapopatiwa kibali;

(b) zisizidi kwa ujumla nusu ya kiasi kilichojumuisha katika makadirio ya matumizi kwa mwaka huo ambayo yaliwasilishwa katika Bunge la Kaunti; na

(c) zijumuishwe, kwenye migao tofauti ya huduma mbalimbali zinazohusiana na pesa zinazotolewa.

Rekebisho la Ibara ya 228 ya Katiba.

**22.** Ibara ya 228 ya Katiba inarekebishwa katika kifungu cha (1) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa” yanayojitokeza punde baada ya maneno “kwa idhini ya” na kuyabadilisha kwa neno “Bunge”.

Rekebisho la Ibara ya 229 ya Katiba.

**23.** Ibara ya 229 ya Katiba inarekebishwa katika kifungu cha (1) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa”

yanayojitokeza punde tu baada ya maneno “kwa idhini ya” na kuyabadilisha kwa neno “Bunge”.

**24.** Ibara ya 233 ya Katiba inarekebishwa katika kifungu cha (2) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa” yanayojitokeza punde tu baada ya maneno “kwa idhini ya” na kuyabadilisha kwa neno “Bunge”.

Rekebisho la Ibara ya 233 ya Katiba.

**25.** Ibara ya 250 ya Katiba inarekebishwa katika kifungu cha (2) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa” yanayojitokeza punde tu baada ya maneno “iliyoidhinishwa na” katika aya ya (b) na kuyabadilisha kwa neno “Bunge”.

Rekebisho la Ibara ya 250 ya Katiba.

**26.** Ibara ya 251 ya Katiba inarekebishwa—

Rekebisho la Ibara ya 251 ya Katiba.

(a) katika kifungu cha (2) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa” yanayojitokeza punde baada ya maneno “anaweza kuwasilisha ardhilhali kwa” na kuyabadilisha kwa neno “Bunge”; na

(b) kwa kufuta maneno “Bunge la Taifa” mwanzoni kwa kifungu cha (3) na kuyabadilisha kwa neno “Bunge”.

## MAELEZO YA MADHUMUNI NA SABABU

Utekelezwaji wa Katiba, hasa utawala wa ugatuzi na bunge la ngazi mbili umepata mafanikio mengi lakini pia umeibua changamoto kadhaa za muundo na mpangilio wa Katiba zinazohitaji mageuzi ili kuimarisha na kudhibiti mfumo wa ugatuzi wa serikali na ili kuwa na umoja na maelewano zaidi katika mfumo huu wa kikatiba.

Sababu kuu ya Mswada huu ni kuimarisha na kulinda ugatuzi. Rasimu ya Mswada huu inajaribu kueleza utaratibu wa kufikia lengo hili kwa–

(a) kufafanua jukumu la vyombo na asasi mbalimbali zinazoanzishwa na Katiba katika mchakato wa ugatuzi;

(b) kuhakiki wajibu wa Seneti na wa Bunge la Taifa ili kufafanua wajibu wa pamoja wa Bunge la Taifa na Bunge la Seneti na majukumu maalum yaliyotengewa kila Bunge;

(c) kuboresha mchakato wa kutunga sheria kulingana na Katiba ili kuhakikisha kwamba Bunge la Taifa na Seneti inatekeleza jukumu fanisi katika mchakato wa kutunga sheria; na

(d) kuhakikisha kwamba Bunge la Taifa na Seneti inatekeleza jukumu fanisi katika mchakato wa kutayarisha bajeti ili kulinda utekelezaji wa ugatuzi.

Mswada huu unapendekeza kurekebisha **Ibara za 94, 95 na ya 96** za Katiba ili kufafanua wazi jukumu la Bunge kwa ujumla na la Bunge la Taifa na la Seneti. Rekebisho hili linanuia kuweka uwazi jukumu la kila Bunge ili kuepuka mwingiliano na fasiri mbalimbali za majukumu ya Bunge la Taifa na ya Seneti.

Mswada huu unapendekeza kurekebisha **Ibara ya 108** ya Katiba ili kuonyesha uongozi na mpangilio wa nyadhifa katika Seneti. Kama ilivyo sasa, Ibara ya 108 ya Katiba inaeleza kuhusu uongozi na mpangilio wa nyadhifa katika Bunge la Taifa na kuacha nje ule wa Seneti.

Mswada huu unapendekeza kurekebisha **Ibara ya 109** ya Katiba ili kutoa nafasi ya kuanzishwa kwa Mswada wowote ama katika Bunge la Taifa au Seneti, isipokuwa Mswada wa kukusanya mapato ya kitaifa unaoweza tu kuanzia kwenye Bunge la Taifa.

Kadhalika, Mswada huu zaidi unaazimia kufutilia mbali **Ibara ya 110** ya Katiba ili kupatia Bunge la Taifa na pia Seneti wajibu kamili wa kutunga sheria. Hali iliyopo sasa imeleta utata kuhusu

jukumu la kutunga sheria la Bunge na maamuzi kadha ya Mahakama hayajaboresha hali hii.

Mswada huu pia unaazimia kurekebisha **Ibara ya 111 na 112** ili kuelezea utaratibu wa Bunge la Taifa na Seneti unaoshughulikia Miswada ya kutenga mapato yaani Mswada wa Ugavi wa Mapato kwa Kaunti, Mswada wa Ugavi wa Mapato ya Ziada kwa Kaunti na Miswada ya kuidhinisha matumizi yaani Mswada wa Kuidhinisha Matumizi na Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada na kutoa nafasi ya utaratibu wa kushugulikia Miswada katika Bunge la Taifa na Seneti.

Rekebisho lililopendekezwa kwa **Ibara ya 113** ya Katiba linahusiana na kuwasilishwa kwa Mswada ili kupatiwa kibali baada ya mchakato wa upatanisho na pia unaondoa Miswada ya ugavi na ya kuidhinisha matumizi kutokana na mchakato wa usuluhishi.

Mswada huu unapendekeza kufutilia mbali **Ibara ya 114** ya Katiba ambayo istilahi "Mswada wa Fedha" umesababisha maana mbali mbali na hatimaye kuzuia michakato ya kutunga sheria katika Seneti.

Rekebisho la **Ibara ya 115** ya Katiba linatoa nafasi ya uwasilishaji wa pamoja wa Mswada unaopitishwa na Bunge na Maspika wa Bunge la Taifa na wa Seneti kwa Rais ili kupata kibali.

Rekebisho la **Ibara ya 116** ya Katiba linatoa ufafanuzi kuhusu kutekelezwa kwa Miswada iliyopatiwa kibali kwa mujibu ya Ibara ya 115(6) ya Katiba.

Mswada huu unapendekeza kurekebisha **Ibara ya 173** ya Katiba kama rekebisho fuatilizi kwa rekebisho la **Ibara ya 221** ya Katiba linalohitaji idhinisho la Bunge la Taifa na Seneti kuhusu makadirio ya Tume ya Huduma za Mahakama.

Mswada huu unapendekeza kurekebisha Katiba ili kuingiza **Ibara mpya ya 199A** ya Katiba ili kutoa nafasi ya kuanzishwa kwa Hazina ya Bunge la Kaunti kwa kila bunge la kaunti.

Mswada huu unapendekeza kurekebisha **Ibara za, 221, 222 na 223** za Katiba ili kutoa nafasi ya utaratibu wa Seneti na Bunge la Taifa wa kuwasilisha na kushughulikia makadirio ya mapato na matumizi ya asasi zilizo katika kiwango cha Serikali ya Kitaifa.

Mswada huu unapendekeza kurekebisha **Ibara ya 224** ya Katiba ili kufafanua kwamba msingi wa utayarishaji wa bajeti wa serikali za kaunti ni Mswada wa Ugavi wa Mapato kwa Kaunti. Mswada huu pia unapendekeza kuingiza vifungu vipya katika Ibara ya 224 vitakavyowezesha serikali za kaunti kupata fedha endapo kutakuwa na uchelewevu katika kupitisha au kuupatia kibali Mswada wa Kugawa Mapato au Mswada wa Ugavi wa Mapato kwa Kaunti.

Mswada huu unapendekeza kurekebisha **Ibara za 157, 215, 228, 229, 233 na 250** za Katiba ili kupatia Bunge la Taifa na Seneti wajibu wa kuwaidhinisha au kuwachunguza Maafisa mbalimbali wa Serikali. Kwa kuambatana na rekebisho lililopendekezwa na **Ibara ya 250** ya Katiba, Mswada huu unapendekeza kurekebisha **Ibara ya 251** ili kupatia Bunge la Taifa na Seneti wajibu wa kumwondoa mamlakani mwanachama wa Tume au afisa wa ofisi huru.

Mswada huu unaelezea utaratibu utakaoimarisha mfumo uliopo wa ugatuzi. Inanuia kufanya hivi kwa kuoanisha majukumu na wajibu wa Bunge kwa njia itakayoendeleza usimamizi bora wa mfumo wa ugatuzi wa serikali. Isitoshe, Mswada huu unapendekeza kubainisha mfumo wa uwajibikaji katika serikali ya kitaifa na serikali za kaunti hasa kuhusiana na utengaji na matumizi ya rasilmali zinazogawiwa serikali ya kitaifa na serikali za kaunti.

Tarehe 22 Julai, 2025.

AARON CHERUIYOT,
*Kiongozi wa Walio Wengi katika Seneti.*

STEWART MADZAYO,
*Kiongozi wa Walio Wachache katika Seneti.*

*Ibara ya 94 ya Katiba inayopendekeza kurekebisha—*

**94. Jukumu la Bunge**

(1) Mamlaka ya kutunga sheria ya Jamhuri yanatokana na wananchi, na katika kiwango cha kitaifa yamo mikonomi mwa na iyanatekeleza.

(2) Bunge linaonyesha uanuai wa taifa, linawakilisha matakwa ya wananchi na linatekeleza uhuru wao wa kujitawala.

(3) Bunge linaweza kuzingatia na kupitisha marekebisho kwa Katiba hii, na kubadilisha mipaka ya kaunti kama inavyoelezwa na Katiba hii.

(4) Bunge litalinda Katiba hii na kuendeleza utawala wa kidemokrasia wa Jamhuri.

(5) Isipokuwa Bunge, hakuna mtu wala chombochenye mamlaka ya kutunga masharti ya kisheria nchini Kenya isipokuwa chini ya mamlaka yanayotolewa na Katiba hii au sheria.

(6) Sheria ya Bunge au sheria ya kaunti inayotoa mamlaka ya kutunga masharti ya kisheria nchini Kenya kwa chombo cha Kitaifa, Afisa wa Serikali au mtu yeyote, kama inavyoelekezwa na kifungu cha (5), itaeleza kwa uwazi nia na malengo yanayotoa mamlaka hayo, mipaka ya mamlaka hayo, aina na mawanda ambayo sheria kama hiyo inaweza kutungwa, na kaida na viwango vinavyohusika katika sheria inayotungwa chini ya mamlaka hayo.

*Ibara ya 95 ya Katiba inayopendekezwa kurekebisha—*

**95. Jukumu la Bunge la Taifa**

(1) Bunge la Taifa linawakilisha watu wa maeneo bunge na maslahi maalum katika Bunge la Taifa.

(2) Bunge la Taifa linajadili na kushughulikia masuala yanayowahusu wananchi.

(3) Bunge la Taifa linatunga sheria kwa kuambatana na Sehemu ya 4 ya Sura hii.

(4) Bunge la Taifa—

(a) linaamua ugavi wa mapato ya kitaifa baina ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti, kama inavyotekelezwa katika Sehemu ya 4 ya Sura ya Kumi na Mbili;

(b) linaidhinisha fedha za matumizi ya serikali ya kitaifa na vyombo vingine vya kitaifa; na

(c) linafanya uangalizi wa mapato ya kitaifa na matumizi yake.

(5) Bunge la Taifa—

(a) hukagua mwenendo wa Rais , Naibu Rais na maafisa wengine wa Serikali kazini na kuanzisha mchakato wa kuwaondoa mamlakani; na

(b) kufanya uangalizi wa vyombo vya Serikali.

(6) Bunge la Taifa huidhinisha matangazo ya vita na kuongeza muda wa hali za hatari.

*Ibara ya 96 ya Katiba ambayo inapendekezwa kufutiliwa mbali—*

**96. Jukumu wa Seneti**

(1) Seneti huwakilisha kaunti na hutumika kulinda maslahi ya kaunti na serikali zake.

(2) Seneti hushiriki katika kuunda sheria za Bunge kwa kuzingatia, kujadili na kuidhinisha Miswada kuhusu kaunti, kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 109 hadi 113.

(3) Seneti huamua mgao wa mapato ya taifa kati ya kaunti, kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 217 na husimamia mapato ya taifa yaliyotolewa kwa serikali za kaunti.

(4) Seneti hushiriki katika usimamizi wa maafisa wa Serikali kwa kuzingatia na kuamua maamuzi yoyote ya kumwondoa Rais au Naibu Rais mamlakani kulingana na Ibara ya 145.

*Ibara ya 108 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**108. Viongozi wa vyama**

(1) Kutakuwa na kiongozi wa chama cha walio wengi na kiongozi wa chama cha walio wachache.

(2) Kiongozi wa chama cha walio wengi atakuwa mtu ambaye ni kiongozi katika Bunge la Taifa wa chama kikubwa zaidi au muungano mkubwa zaidi wa vyama.

(3) Kiongozi wa chama cha walio wachache atakuwa mtu ambaye ni kiongozi katika Bunge la Taifa wa chama cha pili kwa ukubwa au muungano wa pili kwa ukubwa wa vyama.

(4) Mpangilio ufuatao wa ukuu ndio utazingatiwa katika Bunge la Taifa—

(a) Spika wa Bunge la Taifa;

(b) kiongozi wa chama cha walio wengi; na

(c) kiongozi wa chama cha walio wachache

*Ibara ya 109 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**109. Matumizi ya mamlaka ya kutunga sheria**

(1) Bunge litatumia mamlaka yake ya kutunga sheria kupitia Miswada inayopitishwa na Bunge na kupatiwa kibali na Rais.

(2) Mswada wowote unaweza kuanzishwa katika Bunge la Taifa.

(3) Mswada usiohusu serikali za kaunti huzingatiwa tu katika Bunge la Taifa na kupitishwa kulingana na Ibara ya 122 na Kanuni za Kudumu za Bunge la Taifa.

(4) Mswada unaohusu serikali za kaunti unaweza kuanzishwa katika Bunge la Taifa au Seneti na unapitishwa kulingana na Ibara ya 110 hadi 113, Ibara ya 122 na 123 na Kanuni za Kudumu za Mabunge hayo.

(5) Mswada unaweza kuwasilishwa na mbunge yeyote au kamati ya Bunge husika, lakini Mswada wa fedha unaweza kuwasilishwa tu kwenye Bunge la Taifa kulingana na Ibara ya 114.

*Ibara ya 110 ya Katiba ambayo inapendekezwa kufutiliwa mbali—*

**110. Miswada kuhusu serikali ya kaunti**

**(1)** Katika Katiba hii, **"Mswada unaohusu serikali za kaunti"** unamaanisha—

(a) Mswada wenye masharti yanayoathiri majukumu na mamlaka ya serikali za kaunti yaliyoainishwa katika Nyongeza ya Nne;

(b) Mswada unaohusiana na uchaguzi wa wajumbe wa bunge la kaunti au wa mamlaka kuu ya kaunti; na

(c) Mswada uliorejelewa katika Sura ya Kumi na Mbili unaoathiri fedha za serikali za kaunti.

(2) Mswada unaohusu serikali za kaunti ni—

(a) Mswada maalum, utakaozingatiwa chini ya Ibara ya 111, iwapo—

(i) unahusiana na uchaguzi wa wajumbe wa bunge la kaunti au wa kitengo tekelezi cha kaunti; au

(ii) ni Mswada wa kila mwaka wa Ugavi wa Mapato kwa Kaunti uliorejelewa katika Ibara ya 218; au

(b) Mswada wa kawaida, utakaozingatiwa chini ya Ibara ya 112, katika hali nyingine yoyote.

(3) Kabla ya Bunge lolote kuzingatia Mswada, Maspika wa Bunge la Taifa na Seneti wataamua kwa pamoja swali lolote iwapo ni

Mswada unaohusu kaunti, na, iwapo ni hivyo, kama ni Mswada maalum au wa kawaida.

(4) Iwapo Mswada wowote unaohusu serikali za kaunti unapitishwa na Bunge moja, Spika wa Bunge hilo atawasilisha Mswada huo kwa Spika wa Bunge hilo lingine.

(5) Ikiwa Mswada utapitishwa na Bunge la Taifa na Seneta kwa maafikiano, Spika wa Bunge ulipoanzishwa Mswada huo atauwasilisha kwa Rais kwa muda usiozidi siku saba ili upate kibali.

*Ibara ya 111 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**111. Miswada maalum kuhusu serikali za kaunti**

(1) Mswada maalum kuhusu serikali ya kaunti utashughulikiwa kwa namna ile ile kama Mswada wa kawaida kuhusu serikali za kaunti, kwa kuzingatia vifungu vya (2) na (3).

(2) Bunge la Taifa linaweza kurekebisha au kubatilisha Mswada maalum ambao umepitishwa na Seneti kwa uamuzi unaoungwa mkono na angalau thuluthi mbili ya wabunge wa Bunge hilo pekee.

(3) Iwapo uamuzi katika Bunge la Taifa wa kurekebisha au kubatilisha Mswada maalum hautapitishwa, Spika wa Bunge la Taifa atawasilisha, ndani ya siku saba, Mswada huo jinsi ulivyopitishwa na Seneti, kwa Rais ili kupewa kibali.

*Ibara ya 112 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**112. Miswada ya kawaida kuhusu serikali za kaunti**

(1) Iwapo Bunge moja litapitisha Mswada wa kawaida unaohusu kaunti, na Bunge la pili—

(a) lipinge Mswada huo basi utawasilishwa kwa kamati ya usuluhishi iliyo kwa mujibu wa Ibara ya 113; au

(b) lipitishe Mswada huo kwa kuurekebisha, basi utarejeshwa kwa Bunge lililouanzisha kwa ajili ya kushughulikiwa upya.

(2) Ikiwa, baada ya Bunge lililoanzisha Mswada huo kushughulikia upya baada ya kurudishwa kwa mujibu wa kifungu cha (1)(b), Bunge hilo—

(a) litapitisha Mswada kama ulivyorekebishwa, Spika wa Bunge hilo atawasilisha Mswada huo kwa Rais kwa muda usiozidi siku saba ili upate kibali; au

(b) litapinga Mswada kama ulivyorekebishwa, Mswada huo utawasilishwa kwa kamati ya usuluhishi kwa mujibu wa Ibara ya 113.

*Ibara ya 113 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**113. Kamati za usuluhishi**

(1) Iwapo Mswada utatumwa kwa kamati ya mapatanisho kwa mujibu wa Ibara ya 112, Maspika wa Mabunge yote mawili watateua kamati ya usuluhishi yenye idadi sawa ya wajumbe kutoka Bunge la Taifa na Seneti ili kujaribu kuandaa toleo la Mswada huo ambalo litapitishwa na Bunge la Taifa na Seneti.

(2) Iwapo kamati ya usuluhishi itakubaliana kuhusu toleo la Mswada, Bunge la Taifa na Seneti itapiga kura kuidhinisha au kukataa toleo hilo la Mswada.

(3) Iwapo Bunge la Taifa na Seneti itaidhinisha toleo la Mswada lililopendekezwa na kamati ya mapatanisho, Spika wa Bunge la Taifa atawasilisha Mswada huo kwa Rais kwa muda usiozidi siku saba ili upate kibali.

(4) Iwapo kamati ya mapatanisho itashindwa kukubaliana kuhusu toleo la Mswada kwa muda usiozidi siku thelathini, au iwapo toleo lililopendekezwa na kamati litakataliwa na Bunge la Taifa na Seneti, Mswada huo utakuwa umeanguka.

*Ibara ya 114 ya Katiba ambayo inapendekezwa kufutiliwa mbali—*

**114. Miswaada ya Fedha**

(1) Mswada wa fedha hauwezi kushughulika na jambo lolote isipokuwa yale yaliyoorodheshwa katika fasili ya **"Mswada wa fedha"** katika kifungu cha (3).

(2) Iwapo, kwa maoni ya Spika wa Bunge la Taifa, hoja inatoa masharti kwa jambo linalohusu "Mswada wa fedha", Bunge la Taifa litaendelea tu kulingana na mapendekezo ya Kamati husika ya Bunge pekee baada ya kuzingatia maoni ya Waziri husika wa fedha.

(3) Katika Katiba hii, **"Mswada unaohusu masuala ya fedha"** unamaanisha Mswada, isipokuwa Mswada uliobainishwa katika Ibara ya 218, unaojumuisha masharti kuhusu—

(a) ushuru;

(b) uwekaji wa ada kwenye hazina ya umma au marekebisho au kufutiliwa mbali kwa ada hizo;

(c) uidhinishaji, upokeaji, uhifadhi, uwekezaji au utoaji wa fedha za umma;

(d) ukopaji au udhamini wa mkopo wowote au ulipaji wake; au

(e) masuala yanayohusiana na yoyote kati ya masuala hayo.

(4) Katika kifungu cha (3), "ushuru", "fedha za umma" na "mkopo" hazijumuishi ushuru, fedha za umma au mkopo wa kaunti.

*Ibara ya 115 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**115. Kupatiwa kibali au kurejeshwa kwa Mswada kwa Rais**

(1) Kwa muda usiozidi siku kumi na nne baada ya kupokea Mswada, Rais—

(a) atatoa kibali kwa Mswada; au

(b) atarejesha Mswada huo kwa Bunge ili ushughulukiwe upya na Bunge, akieleza kutoridhika kwake kuhusu Mswada huo.

(2) Iwapo Rais atarejesha Mswada kwa ajili ya kushughulikiwa upya, kwa kufuata taratibu zinazofaa chini ya Sehemu hii, Bunge linaweza—

(a) kurekebisha Mswada kwa kuzingatia kikamilifu maoni ya Rais; au

(b) kupitisha Mswada kwa mara ya pili bila marekebisho.

(3) Iwapo Bunge litarekebisha Mswada na kushughulikiwa kikamilifu kwa maoni ya Rais, Spika husika atawasilisha Mswada huo tena kwa Rais ili upate kibali.

(4) Baada ya kuzingatia maoni ya Rais, Bunge linaweza kupitisha Mswada kwa mara ya pili, bila marekebisho, au kwa kufanya marekebisho ambayo hayajashughulikiwa kikamilifu maoni Rais, kwa kupiga kura inayoungwa mkono—

(a) na thuluthi mbili ya wabunge wa Bunge la Taifa; na

(b) thuluthi mbili ya vikoa vya Seneti, iwapo ni Mswada unaohitaji idhini ya Seneti.

(5) Iwapo Bunge limepitisha Mswada chini ya kifungu cha (4)—

(a) Spika husika atauwasilisha tena kwa Rais kwa muda usiozidio siku saba; na

(b) Rais atatoa kibali kwa Mswada huo katika muda usiozidi siku saba.

(6) Iwapo Rais hatatoa kibali Mswada au kurejesha kwa Bunge katika kipindi kilichoainishwa kwenye kifungu cha (1), au kutoa kibali kwa mujibu wa kifungu cha (5)(b), Mswada huo utachukuliwa kuwa umepata kibali baada ya kumalizika kwa kipindi hicho.

*Ibara ya 116 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**116. Kuanza kutumika kwa sheria**

(1) Mswada uliopitishwa na Bunge na kupata kibali cha Rais utachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kama Sheria ya Bunge kwa muda usiozidi saba baada ya kupata kibali.

(2) Kwa kuzingatia kifungu cha (3), Sheria ya Bunge huanza kutumika siku ya kumi na nne baada ya kuchapishwa kwake kwenye Gazeti Ramsi ya Serikali, isipokuwa ikiwa Sheria hiyo itaje tarehe au wakati tofauti itakapo aanza kutumika.

(3) Sheria ya Bunge inayowapa wabunge nyongeza wa fedha ya moja kwa moja haitaanza kutumika hadi baada ya uchaguzi mkuu utakaofuata wa wabunge.

(4) Kifungu cha (3) hakitumiki kwa mafao ambayo wabunge wanapata kama wananchi wa kawaida.

*Ibara ya 157 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**157. Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma**

(1) Kutakuwa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atapendekezwa na Raisi nakuteuliwa rasmi na kwa idhini ya Bunge la Taifa.

(3) Masharti ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma ni sawa na yale ya kuteuliwa kuwa jaji wa Mahakama Kuu.

(4) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atakuwa na mamlaka ya kumuagiza Inspekta Jenerali wa Huduma ya Polisi ya Taifa kuchunguza taarifa au madai yoyote ya mwenendo wa uhalifu na Inspekta Jenerali sharti atii maagizo hayo.

(5) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atahudumu kwa kipindi cha miaka minane na hawezi kuteuliwa tena.

(6) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atatumia mamlaka ya Serikali ya kushtaki na anaweza—

(a) kuanzisha na kuendesha mashtaka ya jinai dhidi ya mtu yeyote mbele ya mahakama yoyote (isipokuwa mahakama ya kijeshi) kuhusiana na kosa lolote analodaiwa kufanya;

(b) kuchukua na kuendeleza mashtaka ya jinai yaliyoanzishwa katika mahakama yoyote (isipokuwa mahakama ya kijeshi) ambayo yameanzishwa au kuendeshwa na mtu au mamlaka nyingine, kwa idhini ya mtu au mamlaka hiyo; na

(c) kwa kuzingatia vifungu vya (7) na (8), kusitisha hatua yoyote kabla ya hukumu kutolewa ya mashtaka yoyote ya jinai iliyoanzishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma au kuendelezwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma chini ya kifungu cha (b).

(7) Iwapo mashtaka yatasitishwa chini ya kifungu cha (6)(c) baada ya upande wa mashtaka kufunga kesi yake, mshtakiwa ataachiliwa huru.

(8) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma hatasitisha mashtaka bila idhini ya mahakama.

(9) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma yanaweza kutekelezwa kibinafsi au kupitia maafisa wa ngazi za chini kulingana na maagizo ya jumla au maagizo maalum.

(10) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma hatahitaji idhini ya mtu au mamlaka yoyote kuanzisha mashtaka ya jinai na katika utekelezaji wa mamlaka au majukumu yake, hatakuwa chini ya mwelekeo au udhibiti wa mtu au mamlaka yoyote.

(11) Katika kutekeleza mamlaka yaliyotolewa na Ibara hii, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atazingatia maslahi ya umma, maslahi ya uendeshaji wa haki na haja ya kuzuia na kuepuka matumizi mabaya ya mchakato wa kisheria.

(12) Bunge linaweza kuunda sheria za kuipatia taasisi zingine mamlaka ya kushtaki mbali na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

*Ibara ya 173 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**173. Hazina ya Mahakama**

(1) Kutakuwa hazina itakayojulikana kama Hazina ya Mahakama ambayo itasimamiwa na Msajili Mkuu wa Mahakama.

(2) Hazina hii itatumika kugharimia usimamizi wa Mahakama na malengo mengine kama yanavyohitajika kwa utekelezaji wa majukumu ya Mahakama.

(3) Kila mwaka wa kifedha, Msajili Mkuu ataandaa makadirio ya matumizi kwa mwaka unaofuata na kuyawasilisha kwa Bunge la Taifa ili yaidhinishwe.

(4) Baada ya makadirio hayo kuidhinishwa na Bunge la Taifa, matumizi ya Mahakama yatatozwa kwa Hazina Kuu na fedha zitatumwa moja kwa moja kwenye Hazina ya Mahakama.

*Ibara ya 215 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**215. Tume ya Ugavi wa Mapato**

(1) Kutakuwa na tume itakayojulikana kama Tume ya Ugavi wa Mapato.

(2) Tume hii itakuwa na watu wafuatao walioteuliwa na Rais—

(a) mwenyekiti, ambaye atateuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge la Taifa;

(b) watu wawili walioteuliwa na vyama vya kisiasa vilivyowakilishwa katika Bunge la Taifa kulingana na idadi ya wabunge wao;

(c) watu watano walioteuliwa na vyama vya kisiasa vilivyowakilishwa katika Seneti kulingana na idadi ya maseneta wao; na

(d) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na fedha.

(3) Watu walioteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha (2) wasio wabunge.

(4) Ili kutimiza masharti ya kuteuliwa kuwa mwanachama wa Tume kwa mujibu kifungu cha (2)(a), (b) au (c), sharti mtu awe na uzoefu mkubwa wa kitaaluma katika masuala ya kifedha na kiuchumi.

*Ibara ya 221 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**221. Makadirio ya bajeti na Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha wa Kila Mwaka**

(1) Angalau miezi miwili kabla ya mwisho wa mwaka wa kifedha, Waziri anayehusika na masuala ya fedha atawasilisha kwa Bunge la Taifa makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kuu kwa mwaka ufuataao wa kifedha ili yawasilishwe katika Bunge la Taifa.

(2) Makadirio yanayorejelewa katika kifungu cha (1)—

(a) yatajumuisha makadirio ya matumizi kutoka Hazina ya Usawazishaji; na

(b) yatakuwa katika muundo, na kulingana na utaratibu, uliowekwa na Sheria ya Bunge.

(3) Bunge la Taifa litazingatia makadirio yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kifungu cha (1) pamoja na makadirio yaliyowasilishwa na Tume ya Huduma za Bunge na Msajili Mkuu wa Mahakama kwa mujibu wa Ibara ya 127 na 173 mtawalia.

(4) Kabla ya Bunge la Taifa kuzingatia makadirio ya mapato na matumizi, kamati ya Bunge hilo litajadili na kukagua makadirio hayo na kutoa mapendekezo kwa Bunge la Taifa.

(5) Katika kujadili na kukagua makadirio hayo, kamati itatafuta maoni kutoka kwa umma na mapendekezo hayo yatazingatiwa wakati kamati inawasilisha mapendekezo yake kwa Bunge la Taifa.

(6) Makadirio ya matumizi ya serikali kuu na makadirio ya matumizi ya Mahakama na Bunge yanapoidhinishwa na Bunge la Taifa, yatajumlishwa katika Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha, ambao utawasilishwa katika Bunge la Taifa ili kuidhinisha fedha kutolewa kutoka kwa Hazina Kuu na kugawa fedha hizo kulingana na majukumu yaliyoorodheshwa katika Mswada.

(7) Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha uliobainishwa katika kifungu cha (6) hautajumuisha matumizi yanayotozwa kutoka kwa Hazina Kuu kulingana na Katiba hii au Sheria ya Bunge.

*Ibara ya 222 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**222. Matumizi kabla ya bajeti ya mwaka kupitishwa**

(1) Iwapo Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha ya mwaka wa kifedha haijapata kibali, au huenda isipate kibali kufikia mwanzo wa mwaka huo wa kifedha, Bunge la Taifa linaweza kuidhinisha fedha kutolewa kutoka kwa Hazina Kuu.

(2) Fedha zilizotolewa kwa mujibu wa kifungu cha (1)—

(a) zitatumika kwa malengo ya kugharimia matumizi yanayohitajika ili kuendeleza huduma za serikali kuu katika mwaka huo hadi wakati Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha itakapopata kibali;

(b) zisizidi jumla ya nusu ya kiasi kilichojumuishwa katika makadirio ya matumizi ya mwaka huo yaliyowasilishwa kwenye Bunge la Taifa; na

(c) zijumlishwe, chini ya migao tofauti kwa huduma mbalimbali ambazo fedha hizo zilitolewa, katika Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha.

*Ibara ya 223 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**223. Kuidhinisha matumizi ya ziada ya fedha**

(1) Kwa kuzingatia masharti ya vifungu vya (2) hadi (4), serikali kuu inaweza kutumia fedha ambazo hazijaidhinishwa iwapo—

(a) kiasi kilichoidhinishwa kwa malengo fulani kwa mujibu wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha hakitoshi au mahitaji ya matumizi yamejitokeza kwa lengo ambalo halina kiasi kilichoidhinishwa na sheria hiyo; au

(b) fedha zimetolewa kutoka Hazina ya Dharura.

(2) Idhini ya Bunge kwa matumizi yoyote chini ya Ibara hii itafutwe katika muda usizidi miezi miwili baada ya fedha kutolewa kwa mara ya kwanza, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha (3).

(3) Iwapo Bunge halina kikao katika kipindi kilichobainishwa kwa mujibu wa kifungu cha (2), au limekuwa na kikao lakini kikaahirishwa kabla ya idhini kuombwa, basi idhini itaombwa katika muda usiozidi ya wiki mbili baada ya vikao kurejea.

(4) Bunge la Taifa litakapoidhinisha matumizi chini ya kifungu cha (2), Mswada wa kuidhinisha matumizi ya fedha utawasilishwa kwa ajili ya kuidhinishwa kwa fedha zilizotumika.

(5) Katika mwaka wowote wa kifedha, serikali kuu haitatumia kwa mujibu wa ibara hii zaidi ya asilimia kumi ya jumla ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka huo wa kifedha, isipokuwa, kwa hali maalum, Bunge liidhinishe asilimia ya juu zaidi.

*Ibara ya 224 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**224. Miswada ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha za Kaunti**

Kwa kuzingatia Mswada wa Kugawa Mapato uliopitishwa na Bunge chini ya Ibara ya 218, kila serikali ya kaunti itaandaa na kupitisha bajeti yake ya mwaka na Mswada wa kuidhinisha matumizi ya fedha kwa muundo, na kulingana na utaratibu, uliowekwa na sheria ya Bunge.

*Ibara ya 228 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**228. Mdhibiti wa Bajeti**

(1) Kutakuwa na Mdhibiti wa Bajeti ambaye atapendekezwa na Rais na, kwa idhini ya Bunge la Taifa, kuteuliwa rasmi na Rais.

(2) Ili mtu atimize masharti ya kuwa Mdhibiti wa Bajeti, sharti awe na ujuzi mpana wa fedha za umma au angalau uzoefu wa miaka kumi katika ukaguzi wa usimamizi wa fedha za umma.

(3) Mdhibiti wa Bajeti, kulingana na Ibara ya 251, atahudumu kwa kipindi cha miaka minane na hawezi kuteuliwa tena.

(4) Mdhibiti wa Bajeti atasimamia utekelezaji wa bajeti za serikali kuu na serikali za kaunti kwa kuidhinisha utoaji wa fedha za umma kwa mujibu wa Ibara za 204, 206 na 207.

(5) Mdhibiti wa Bajeti hataidhinisha utoaji wowote wa fedha za umma isipokuwa ikiwa ameridhika kuwa utoaji huo umeidhinishwa na na sheria.

(6) Kila baada ya miezi minne, Mdhibiti wa Bajeti atawasilisha kwa ripoti kuhusu utekelezaji wa bajeti za serikali kuu na za kaunti Bunge la Taifa na Seneti.

*Ibara ya 229 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**229. Mkaguzi Mkuu**

(1) Kutakuwa na Mkaguzi Mkuu ambaye atapendekezwa na Rais na, kwa idhini ya Bunge la Taifa, kuteuliwa rasmi na Rais.

(2) Ili mtu atimize masharti ya kuwa Mkaguzi Mkuu, sharti awe na ujuzi mpana wa fedha za umma au angalau uzoefu wa miaka kumi katika ukaguzi au usimamizi wa fedha za umma.

(3) Mkaguzi Mkuu atahudumu, kulingana na Ibara ya 251, kwa kipindi cha miaka minane na hawezi kuteuliwa tena.

(4) Ndani ya miezi sita baada ya kukamilika kwa kila mwaka wa kifedha, Mkaguzi Mkuu atakagua na kuwasilisha ripoti, kuhusiana na mwaka huo wa kifedha, kuhusu—

(a) hesabu za serikali kuu na za kaunti;

(b) hesabu za hazina zote na mamlaka za serikali kuu na za kaunti;

(c) hesabu za mahakama zote;

(d) hesabu za tume na ofisi zote huru zilizoanzishwa na Katiba hii;

(e) hesabu za Bunge la Taifa, Seneti na mabunge ya kaunti;

(f) hesabu za vyama vya kisiasa vinavyofadhiliwa kwa kutumia fedha za umma;

(g) deni la umma; na

(h) hesabu za taasisi nyingine yoyote ambayo sheria inahitaji ikaguliwe na Mkaguzi Mkuu.

(5) Mkaguzi Mkuu anaweza kukagua na kuwasilisha ripoti kuhusu hesabu za taasisi yoyote inayofadhiliwa na fedha za umma.

(6) Ripoti ya ukaguzi itathibitisha iwapo fedha za umma zimetumika kihalali na kwa njia yenye ufanisi.

(7) Ripoti za ukaguzi zitawasilishwa Bunge au katika bunge la kaunti husika.

(8) Katika muda usiozidi miezi mitatu baada ya kupokea ripoti ya ukaguzi, Bunge au bunge la kaunti litajadili na kuzingatia ripoti hiyo na kuchukua hatua mwafaka.

*Ibara ya 233 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**233. Tume ya Utumishi wa Umma**

(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi wa Umma.

(2) Tume ya Utumishi wa Umma itakuwa na mwenyekiti, makamumwenyekiti na wajumbe wengine saba watakaoteuliwa na Rais kwa idhini ya Bunge la Taifa.

(3) Kulingana na kifungu cha (4), mtu hawezi kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume ikiwa—

(a) amewahi, kwa wakati wowote ndani ya miaka mitano iliyopita, kushikilia wadhifa, au kugombea nafasi kama—

(i) mbunge au wa mjumbe was bunge la kaunti; au

(ii) mjumbe wa baraza la uongozi la chama cha kisiasa; au

(b) anashikilia wadhifa wowote katika serikali;

(c) ni, au amewahi kuwa kwa wakati wowote, mgombea katika uchaguzi kama munge au mjumbe wa bunge la kaunti; au

(d) anashikilia, au amewahi kwa wakati wowote, kushikilia wadhifa katika shirika lolote la kisiasa linalofadhili au kusaidia, au limewahi kufadhili au kusaidia, mgombea wa uchaguzi kama Bunge au mjumbe wa bunge la kaunti.

(4) Kifungu cha (3)(c) na (d) kitaacha kutumika kwa mtu baada ya chaguzi kuu mbili za Bunge kufanyika tangu mtu huyo aache kuwa mgombea au mwenye wadhifa huo.

(5) Kutakuwa na katibu wa Tume hiyo.

(6) Katibu—

(a) ndiye mtendaji mkuu wa Tume; na

(b) atateuliwa na Tume kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena mara moja.

*Ibara ya 250 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**250. Uanachama, uteuzi na masharti ya kuhudumu**

(1) Kila tume itakuwa na angalau wanachama watatu, lakini hawatazidi wanachama tisa.

(2) Mwenyekiti na kila mjumbe wa tume, na anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru—

(a) atatambuliwa na kupendekezwa kuteuliwa kwa njia iliyoainishwa na sheria ya kitaifa;

(b) ataidhinishwa na Bunge la Taifa; na

(c) atateuliwa na Rais.

(3) Ili kuteuliwa, sharti mtu awe ametimiza masharti mahususi yanayohitajika na Katiba hii au sheria ya kitaifa.

(4) Uteuzi wa wajumbe wa tume na ofisi huru utazingatia maadili ya kitaifa yaliyoorodheshwa katika Ibara ya 10 na kanuni kwamba muundo wa tume na ofisi, kwa jumla, sharti uonyeshe maeneo na makabila mbalimbali ya watu wa Kenya.

(5) Kamishna anaweza kuhudumu akifanya kazi ya muda.

(6) Kamishna au anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru,—

(a) isipokuwa akiwa ni kutokana na wadhifa wake, atateuliwa kwa kipindi kimoja cha miaka sita na hawezi kuteuliwa tena; na

(b) isipokuwa akiwa ni kutokana kutokana na wadhifa wake, au kamishna wa muda, hatashikilia ofisi nyingine yoyote au ajira yenye faida, iwe ya umma au kibinafsi.

(7) Malipo na mafao yanayolipwa Kamishna au kwa ajili yake au mtu anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru yatatozwa kwa Hazina Kuu.

(8) Malipo na mafao yanayolipwa kamishna, au kwa ajili yake, au mtu anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru hayatabadilishwa kwa njia isiyomfaa kamishna huyo au mtu anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru.

(9) Mjumbe wa tume, au mtu anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru, hatachukuliwa hatua ya kisheria na wajibu wa kisheria kuhusu jambo lolote alilofanya kwa nia njema katika utekelezaji wa jukumu la ofisi.

(10) Makamishna watamchagua makamu mwenyekiti miongoni mwao—

(a) katika kikao cha kwanza cha tume; na

(b) kila inapohitajika kujaza nafasi katika wadhifa wa makamu mwenyekiti.

(11) Mwenyekiti na makamu mwenyekiti wa tume hawapaswi kuwa wa jinsia moja.

(12) Kutakuwa na Katibu kwa kila tume ambaye—

(a) atateuliwa na makamishna; na

(b) afisa mtendaji mkuu wa tume.

*Ibara ya 251 ya Katiba ambayo inapendekezwa kurekebishwa—*

**251. Kuondolewa mamlakani**

(1) Kamishna (isipokuwa akiwa ni kutokana na wadhifa wake), au anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru, anaweza kuondolewa mamlakani tu kwa sababu za—

(a) ukiukaji mkubwa wa Katiba hii au sheria nyingine yoyote, ikiwemo kukiuka Sura ya Sita;

(b) utovu mkubwa wa nidhamu, katika utendaji wa majukumu ya kamishna au anayeshikilia wadhifa au vinginevyo;

(c) udhaifu wa kimwili au kiakili wa kutekeleza majukumu ya kazi;

(d) kutokuwa na uwezo; au

(e) kufilisika.

(2) Mtu ambaye angependa mjumbe wa tume au mtu anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru aondolewe kazini kwa misingi iliyoorodheshwa katika kifungu cha (1) anaweza kuwasilisha ardhilhali kwa Bunge la Taifa akionyesha ukweli unaodaiwa kuunda msingi huo.

(3) Bunge la Taifa litashughulikia ardhilhali hiyo na likiridhika kwamba lina msingi kwa mujibu wa kifungu cha (1), litatuma ardhilhali hiyo kwa Rais.